

[R5929]

AMANI MIONGONI MWENU

SOTE tumewai kusikia methali isemayo, "Alimasi hukata Alimasi." Vito vyote huwa vigumu sana na hali kadhalika safi sana. Ugumu huu huongeza thamani yao. Watu wa Bwana wote ni vito - hawajatakaswa tu kwa neema ya Bwana, lakini wana tabia angavu kabisa. Huu ukiwa ndio ukweli wa mambo, kama tulivyoonyesha hapo awali, kuna hatari zaidi ya kukata na kukwaruza wanapokuwa pamoja kuliko vile vifaa hivyo vingekuwa si vigumu sana kiasi hicho. Puti na udongo haukati - wala tabia ya ubora kama wa puti.

Tukikumbuka hili, watu wa Bwana wanapaswa kuhurumiana na kuthaminiana sana. Tunajifunza kuthamini, kama Bwana anavyofanya, tabia njema, tabia yenye nguvu, lengo imara, ingawa wakati mwingine ubora huu wa tabia unaweza kusababisha shida. Si ajabu basi Madarasa ya Biblia ya Waberoya huwa na shida wakati mwingine, kama vile mashirika ya kilimwengu!

WATU WA BWANA SIO WAKUZA UGOMVI

Hata hivyo, watu wa Bwana wanapaswa kukumbuka maagizo maalum ya Yesu Kristo kuwa wawe waleta amani na sio wakuza ugomvi. Haihitaji ustadi mkubwa kuchochea shida. Inahitaji upole, uungwana, uvumilivu, na sifa zingine za Roho Takatifu miongoni mwa watu wa Bwana kuzuia ugomvi, hata kama nia nzuri ipo. Twafaa kuwa macho asije Adui akatujaribu, na kutupotosha kutoka kwa njia za amani!

Inahitaji uzoefu mkubwa na hekima inayotoka juu ili kutuwezesha kutoa uamuzi ulio sawa ikiwa suala la utofauti kati ya wengine na sisi ni suala la kanuni, ambapo ukweli wa kimsingi uko hatarini, au ikiwa ni swali la maoni tu na kupendekeza bila kuhusisha kanuni. Katika uamuzi wa baadaye, tunapaswa kuwa tayari kuondoa pingamizi lolote lile kwa ajili ya amani, wakati ambapo hatungefanya hivyo kama tungehusisha misimamo ya kanuni. Walakini, udanganyifu mara nyingi huwasilishwa kwetu kwamba mapendekezo yetu daima huungwa mkono na kanuni za ukweli na haki. Lazima tujifunze kutokana na uzoefu kwamba hili ni kosa, na lazima tuchunguze kwa umakini kila shauri kama hilo, tupate hekima ya Bwana kutuwezesha kuona tofauti kati ya lile ambalo ni pendekezo letu tu na masuala hayo ambayo yanajumuisha kanuni na mafundisho ya asili ya Kiungu.

Kwa mfano, katika Darasa kuna ndugu au dada ambao husisitiza sana juu ya jambo linalofanyika kwa njia fulani, kwa sababu hilo limekuwa kama desturi ya awali au kwa sababu wanaamini kuwa ndiyo njia bora. Wako tayari kuhimiza ugomvi kama pendekezo lao halifuatwi. Njia ya busara zaidi ni kuachilia mbali pendekezo letu kwa kupendelea pendekezo la wengine, ikiwa wanasisitiza, alimradi pana matokeo mwafaka yatakayofikiwa — yaani, mradi matakwa ya Darasa yamepatikana hasa; kwa kuwa matakwa ya Darasa yanapaswa kuchukuliwa kama

mapenzi ya Bwana - au ikiwa si hivyo, Bwana atabatilisha suala hilo na kutuletea funzo kutokana nalo katika Darasa.

Kila mmoja wa washiriki wa Darasa anapaswa kujitahidi sana kukuza katika Darasa matunda ya Roho Takatifu - upole, uungwana, uvumilivu, fadhili za kindugu, upendo, furaha, amani. Kukuza huku kunapaswa kufanywa kwa kukumbuka sifa hizi na kuzitumia sisi wenyewe, na hivyo kutoa mfano kwa wengine na kuonyesha ushawishi wa Roho Takatifu anayefanya kazi ndani ya mioyo na maisha yetu.

KOSA LA MARA KWA MARA

Aghalabu, kosa hufanywa la kufikiria kwamba uzito wote wa uwajibikaji u juu yetu — tukisahau kwamba jukumu letu linakoma tunapotumia uamuzi wetu na kuutekeleza.

Ukosefu wa imani katika Bwana unahusishwa kwa karibu na kosa la kuleta ugomvi katika Darasa kwa mbinu fulani. Tunapaswa kukumbuka shauku ya Bwana katika Darasa na kwa watu Wake wote, na kwamba Ana uwezo na yu tayari kubatilisha uzoefu wetu kabisa — vivyo hivyo uzoefu wa wengine. Ikiwa, basi, mambo hayaendi haswa kama tupendavyo Darasani, itakuwa bora kwetu, na mara nyingi kwa wote, kwamba tupeleke jambo hilo kwa Bwana katika sala, badala ya kusumbua na kulaumu kila wakati kile kilicho au kinachoonekana kuwaridhisha wengine, au angalau kwa walio wengi katika Darasa.